BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

OROHDA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 09 Juni, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

78. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa vijana wenye ulemavu wana haki sawa na vijana wasio na ulemavu.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha vijana wenye ulemavu wanajengewa uwezo juu ya masuali mbali mbali ya kijamii ili waweze kunufaika na fursa za vijana zilizopo.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

242. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Changamoto ya uchafu ni tatizo kubwa linaloikumba visiwa vyetu vya Zanzibar na inaondosha haiba ya mji wa Zanzibar. Hali hii inapelekea kuwakimbiza watalii kuitembelea nchi yetu.

(a) Je, Wizara yako ina nafasi gani ya kuifahamu changamoto hiyo.
(b) Ni ipi mikakati ya Wizara yako ya kuuweka Mji wa Zanzibar katika mazingira mazuri na yenye kuvutia.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

211. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kivipi malalamiko ya haki, ustawi, heshima na utu kwa wafanyakazi wa mahoteli dhidi ya waajiri wao yamekuwa yakipungua siku hadi siku.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

46. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Benki Kuu kupitia sekta ya kifedha nchini imehamasisha utumiaji wa huduma ya mtandao (digital) katika kurahisisha kupatikana huduma kwa wananchi. Pamoja na upokeaji nzuri wa huduma hii kwa wananchi, zipo lawama kwamba benki kupitia mashine za malipo kwa wafanyabiashara (Point of sale au POS) zinatoa ada kubwa kwa watumiaji kinyume na taratibu zilizopo.

(a) Je, ni upi muongozo wa utozaji ada (charges) ya kutumia kadi za kibenki katika mashine za POS.

(b) Kupitia muongozo wa BOT, ni upi ukomo wa kiwango cha fedha za muamala wa kidijital ambazo mteja anaweza kufanya kwa siku.

(c) Kwa takwimu zilizopo ni miamala mingapi inayotumia POS hufanyika Zanzibar kwa mwezi tokea huduma hii kuanza.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

65. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kuna maeneo mbali mbali ambayo Serikali imesambaza miundombinu ya maji na kuweka mabomba mapya na baadhi kupita katika mashamba ya wananchi na kupelekea vipando vyao kuharibika.

Je, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia zao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

89. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuwasaidia wakulima kwa kuwapatia mbolea ili waweze kulima kwa wepesi na kupata mazao mengi na yaliyo bora.

(a) Je, ni tani ngapi za mbolea wamepatiwa wakulima kwa mwaka huu.

(b) Kwa kiasi gani kumekuwa na unafuu katika bei za ununuzi wa mbolea hizo.

268. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi ambao kilimo chao huathiriwa sana na maji ya chumvi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

205. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamatuni na Michezo:

(a) Kwa sasa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) lina wataalamu wangapi wabobevu katika fani za teknolojia ya habari na dijitali.

(b) Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) linajipanga vipi kusomesha wataalamu mahususi ili kuenda sambamba na mabadiliko ya kiteknolojia ya habari siku hadi siku.

**Wizara ya Afya:**

102. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hali halisi ya kutokomeza ugonjwa wa kichocho inachukua sura gani kwa sasa.

## Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

26. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa muda mrefu, wananchi wa Pemba wamekuwa wakiomba Serikali kupitia Wawakilishi wao kuwafikishia ombi la kupatiwa huduma ya ndege kupitia Shirika la Ndege la Tanzania. Pamoja na kutolewa ahadi za mara kwa mara kwamba Shirika hilo lingeanza safari zake kuelekea Pemba, bado ahadi hizo hazijatekelezwa.

(a) Je, ni abiria wangapi hutumia Kiwanja cha Ndege cha Pemba kwa mwaka.

(b) Ni changamoto zipi zimeifanya Shirika la Ndege la Tanzania kushindwa kufanya safari za ndege kuelekea Pemba.

(c) Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kuja na mkakati wa kuanzisha shirika lake la ndege.

311. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imefanya kazi nzuri ya kuweka alama maalumu za barabarani kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu. Hata hivyo, alama hizo zimeharibiwa kwa kuangushwa katika maeneo mbali mbali nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzirejesha upya alama hizo ili Watu Wenye Ulemavu waweze kutumia barabara zetu kwa usalama.

## Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda :

260. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Uwepo wa viwanda mbali mbali hapa Zanzibar utapunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kupunguza bei za bidhaa hizo na kuongeza ajira kwa vijana.

Je, ni viwanda vingapi vipya vimeanzishwa katika kipindi hiki cha miaka mitano.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

36. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Walimu Wakuu na Wasaidizi wao wanafanya kazi kubwa ya kufanikisha maendeleo ya skuli wanazoziongoza hapa Zanzibar. Pamoja na juhudi hizo kumekuwa na malalamiko kutoka kwa walimu juu ya posho ya madaraka wanayotakiwa kupewa kwa kazi wanayoifanya.

(a) Je, ni upi waraka unaozungumzia masuala ya posho kwa walimu hawa na kiasi gani wanatakiwa kupewa kwa mwezi.

(b) Je, ni ipi hali ya utoaji wa posho hii kwa walimu hawa wanaofanya kazi kwa juhudi kubwa.

(c) Je, tathmini inaonesha ni walimu wangapi wenye cheo hicho wanastahiki kupata posho hiyo kwa skuli za msingi na sekondari.

277. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza kwa dhati Serikali yetu kwa ujenzi wa miundombinu ya elimu, ujenzi wa skuli mpya na ukarabati wa madarasa.

Ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha skuli zetu zinakuwa na miundombinu ya maji safi na salama ili kulinda afya za walimu na wanafunzi wetu.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

236. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kuna malalamiko ya kuibuka magonjwa ya mwani ambayo bado hayajajulikana tiba yake.

(a) Vipi suala hili linatambuliwa na Wizara yako.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kuhakikisha inayaondoa magonjwa hayo.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Zahanati ya Kale (Old Dispensary) ina mchango gani katika historia ya Zanzibar.

270. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa katika eneo la Mgagadu ipo miembe ya kumbukumbu ambayo ni moja ya ukumbusho kwa vizazi vyetu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulienzi eneo hilo.

**Zanzibar,**
**09 Juni, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR</u>**